

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME-SHULE YA SEKONDARI YA MVUREKONGEI
S.L.P 276-SAME

15 DESEMBA, 2021.

Kumb. Na MVKSS/E10/23/VOL 1/2021/01

MZAZI WA.....

S.L.P.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MVUREKONGEI WILAYA YA SAME MKOA
WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Mhula wa kwanza wa Masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2.1 SARE YA SHULE,

a) Sare za shule hii kwa wavulana ni:

- (i) Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi aina ya tomato
- (ii) Suruali mbili (2) rangi ya light blue moja(1) na damu ya mzee moja(1)
- (iii) Viatu vyeusi vya kufunga kamba visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeusi pea mbili (2)
- (v) Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi
- (vi) Nguo za Michezo -Bukta nyekundu na T-Shirt ya blue
- (vii) Sweta la dark blue

NB (i) Suruali zishonwe pana za kutosha zenye marinda mawili za kuvaliwa kiunoni na sio mlegezo.

(ii) Sare ya shule hii ni suruali ya heshima yenye mkunjo chini "turn up"

b) Sare za Shule hii kwa Wasichana ni,

- (i) Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi aina ya tomato
- (ii) Sketi mbili (2) rangi ya light blue moja(1) na damu ya mzee moja(1)
- (iii) Sweta la dark blue
- (iv) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visivyo na visigino virefu,
- (v) Soksi nyeusi pea mbili (2).
- (vi) Nguo za michezo –Bukta blue na t-shirt ya blue

c) Rangi ya Hijab ifanane na sare ya Shule

d) Daftari Counter Book Quire two tisa (9) kulingana na idadi ya Masomo, kalamu na mkebe wa Hisabati

e) Kamusi ya Kiswahili na Kiingereza

2.2 CHAKULA

Chakula cha Mchana ni jukumu la Mzazi/Mlezi. (Utaratibu wa chakula kinapokelewa na Kamati ya Wazazi).

2.3 Vifaa vya usafi (Ndoo ndogo 1 na ufagio wa chelewa 1)

2.4 Matibabu: Kila mzazi atagharamikia matibabu ya mwanae

NB: Siku ya kufungua Shule Mzazi/Mlezi aje na mwanae.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mijiibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla nijambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kwa kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote na
- h) Kutunza mali za Umma..

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi,Cocaine,Mirungi,Kubeli na kadhalika.
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma,
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa,
- (h) Kuwa mjamzito(Kusababisha Mimba/Kusababisha Mimba
- (i) Kuoa au Kuolewa,
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi,
- (m) Kuwa na Simu ya mkononi
- (n) Kushiriki tukio lolote la sherehe za usiku(Mwisho saa kumi na mbili jioni)
- (o) Udanganyifu katika mitihani mbalimbali inayofanywa hapa shuleni.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Serikali na Form itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni (Form imeambatanishwa)
- (b) Form ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika migomo,Utoro (Ukishaandikishwa huruhusiwi kuacha Shule),Fujo na Makosa ya Jinai (Form imeambatanishwa).
- (c) Form ya mzazi/mlezi ya kukiri kukubaliana na sheria na maelekezo yatakayotolewa na shule

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

.....

MKUU WA SHULE

